

Swahili - The IRS Warns of Consequences when a Taxpayer Uses an Unskilled or Unscrupulous Tax Preparer (5-19-2011)

## **IRS Wanaonya madhara kwa Mlipakodi anapotumia Waandalizi wa Kodi ambao hawana ujuzi au wasio na maadili (5-19-2011)**

IRS Uchunguzi wa makosa ya Jinai (CI) inakukumbusha;

- Walipakodi wanawajibika kwa usahihi wa maingizo yote yanayofanyika kwenye marejesho yao ya kodi, ambayo yanajumuisha ratiba zinazohusiana, fomu na nyaraka nyingine. Hii itabaki kuwa kweli hata kama rejesho limeandaliwa na mlipakodi au mwandalizi wa marejesho.
- Kuwa mwangalifu katika kuchagua mtaalamu wa kodi ambaye ataandaa marejesho yako. Baadhi ya dondoo za msingi na mwongozo kuwasaidia walipakodi katika kuchagua wataalamu wa kodi wenye sifa ni:
  - **Epuka waandalizi wa marejesho ambao wanadai wanaweza kupata malipo mengi kuliko waandalizi wengine.**
  - Epuka waandalizi ambao ada zao zinategemea asilimia ya kiasi cha pesa za malipo.
  - Tumia wataalamu wenye sifa ambao wanasaini na kuingiza namba ya kitambulisho cha mwandalizi wa kodi (PTIN) kwenye marejesho ya kodi na wanakupatia nakala kwa ajili ya kuweka kumbukumbu..
  - Zingatia kama mtu binafsi au kampuni itakuwepo kujibu maswali kuhusu maandalizi ya marejesho yako ya kodi, miezi, hata miaka, baada ya marejesho kutumwa.
  - Kamwe usisaini fomu ya kodi ambayo haina kitu.
  - Uliza maswali. Unamfahamu mtu yeyote ambaye amemtumia mtaalamu wa kodi? Waliridhishwa na huduma waliyoipata?
- Kukwepa kodi ni uhalifu, kosa la jinai, adhabu ni hadi miaka 5 jela na faini ya dola za Kimarekani 250,000.

Ukiwa na shaka, angalia! Walipakodi wanasikia malalamiko kutoka kwa waandalizi wanaorejesha malipo makubwa kuliko waandalizi wengine wamehimizwa kuangalia kwa wataalamu wa kodi walio waaminifu au IRS kabla ya kujihusisha.